Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**NIYONZIMA AIGUSTINE DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 058/2016**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**TAREHE 13 JUNI 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Juni 2023**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), leo, imetoa Hukumu katika kesi ya *Niyonzima Augustine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

*Niyonzima Augustine* (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Rwanda. Wakati wa kuwasilisha maombi haya, alikuwa akitumikia kifungo cha miaka thelathini (30) katika Gereza Kuu la Butimba, baada ya kukutwa na hatia ya ubakaji. Alidai kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi), alikiuka haki zake zilizohakikishwa chini ya Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba na Kifungu cha 13 cha Katiba ya Mjibu Maombi kuhusiana kesi zinazoendeshwa kwenye mahakama ya ndani.

Kuhusiana na mamlaka ya kisheria, Mjibu Maombi aliweka pingamizi kuhusu mamlaka ya kisheria ya mahakama kwa sababu mbili. Kwanza, kwamba Mahakama hii haijapewa uwezo wa kutathmini masuala ya ushahidi yaliyotolewa wakati wa kesi ya Mwombaji mbele ya mahakama za ndani. Pili, kwamba Mahakama hii haiwezi kukaa kama mahakama inayoendesha kesi au ya rufaa kwa maswala ambayo yako ndani ya mamlaka ya mahakama za ndani.

Mahakama ilirejelea kwamba chini ya Kifungu cha 3(1) cha Itifaki, ina mamlaka ya kuchunguza kesi zinazohusu tafsiri na matumizi ya Mkataba na ina uwezo wa kuchunguza kesi za mahakama za ndani ili kuamua endapo ziliendeshwa kwa mujibu wa Mkataba. Kwa kuzingatia kwamba Maombi ya sasa yanadai ukiukaji wa Mkataba kuhusiana na kesi za ndani, Mahakama ilibaini kwamba ina mamlaka ya kisheria na kwa hivyo ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi.

Ingawa pande zote mbili hazikuweka pingamizi kuhusu mamlaka yake ya muda, binafsi na ya kieneo, hata hivyo, Mahakama ilichunguza vipengele hivi vya mamlaka yake na kuthibitisha kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi.

Kuhusu ukubalifu wa Maombi, Mahakama, ilizingatia mapingamizi mawili (2) yaliyoibuliwa na Mjibu Maombi, yanayohusiana, kwanza, na matakwa ya kukamilisha taratibu zote za ndani, na, pili, kuhusu muda ambao Maombi yaliwasilishwa baada ya kukamilika taratibu za ndani.

Kuhusu matakwa ya kukamilisha taratibu zote za ndani, Mahakama iliona kwamba katika Maombi haya, madai ya Mleta Maombi huunda sehemu ya "kifungu cha haki na dhamana" zinazohusiana na haki ya kuendesha kesi kwa misingi ya haki iliyosababisha rufaa hii. Aidha, Mahakama hii inaona kwamba Mjibu Maombi alikuwa na fursa ya kushughulikia uwezekano wa uvunjaji wa haki za binadamu mbele ya mahakama za ndani lakini hakufanya hivyo. Kuhusu kuwasilisha ombi la kikatiba mbele ya Mahakama Kuu ya Mjibu Maombi, kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 13 cha Katiba ya Mjibu Maombi, Mahakama imerudia kusema kwamba njia hii, katika mfumo wa mahakama wa Tanzania, ni njia isiyo ya kawaida ambayo Mleta Maombi hatakiwi kuipitia kabla ya kufikia Mahakama hii. Kwa hiyo, Mahakama inaona kwamba Mleta Maombi alitumia njia zote za ndani kama ilivyonyeshwa chini ya Kifungu cha 56(5) cha Mkataba na Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama na kwa hivyo, inatupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi.

Kuhusu pingamizi la kushindwa kuwasilisha Maombi ndani ya muda unaofaa baada ya kukamilisha taratibu zote za ndani, Mahakama imesisitiza tena uamuzi wake kwamba tathmini ya ufaafu wa muda hutegemea mazingira fulani ya kila kesi na unapaswa kuamuliwa kwa kuangalia kila kesi kivyake. Katika kesi hii, Mahakama inaona kwamba muda wa kuwasilisha Maombi, yaani, ambao ulikuwa miezi tisa (9) na siku nane (8) ni muda unaofaa.

Kwa misingi hiyo, Mahakama ilizingatia endapo Mleta Maombi alikiuka haki za Mjibu Maombi, kwa kuchunguza madai manne (4) yaliyotolewa na Mleta Maombi, ambayo ni: (i) madai kwamba hakupewa usaidizi wa sheria bila malipo; (ii) madai ya kushindwa kuuarifu Ubalozi wa Rwanda nchini Tanzania kuhusu kukamatwa na kufungwa kwa Mleta Maombi; (iii) madai ya kushindwa kuzingatia ushahidi; na mwisho, (iv) madai kwamba kesi hiyo haikuthibitishwa bila shaka yoyote.

Kuhusu madai ya kushindwa kutoa msaada wa kisheria bila malipo, Mjibu Maombi alisema kuwa sheria za Tanzania hazitoi uwakilishi wa kisheria wa lazima au wa moja kwa moja kwa wale wanaoshtakiwa kwa kosa la ubakaji. Aidha, mtuhumiwa ambaye anahitaji uwakilishi wa kisheria bila malipo lazima aombe

kupewa msaada wa kisheria na kila ombi linapimwa kivyake. Aidha, kesi mbele ya mahakama za ndani hazikuonyesha kwamba Mleta Maombi alihitaji msaada wa kisheria na, kwa hali yoyote, msaada wa kisheria unapatikana katika Mahakama ya Rufaa kwa mujibu wa sheria za Mleta Maombi. Mjibu Maombi anapinga madai ya Mleta Maombi, kwa kuwa Serikali daima inawachukulia watu wake wote kuwa sawa mbele ya sheria, na kuwapa haki bila ubaguzi, haki zao zinahamasishwa na kulindwa mbele ya sheria kwa usawa kabisa.

Mleta Maombi anasema kwamba amejizatiti kulinda haki za binadamu kama ilivyoelezwa chini ya Mkataba na ametekeleza na kupitisha hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria (Kesi za Jinai) Sura ya 21 ya Sheria zinazotoa msaada wa kisheria bila malipo katika kesi za jinai zinazohusisha watu ambao ni masikini, ambayo ilitungwa wakati ambapo kesi ya jinai ilifunguliwa dhidi ya Mleta Maombi.

Mahakama hii iliona kwamba, kwa kuzingatia kwamba Mleta Maombi ni raia wa kigeni, maskini na kwa sababu ya ukubwa wa adhabu iliiyotolewa kulingana na kosa, lilikuwa ni suala la haki kumpatia Mleta Maombi usaidizi wa kisheria bila malipo. Aidha, Mjibu Maombi ana wajibu wa kutoa msaada wa kisheria bila malipo na bila kujali iwapo mtuhumiwa ameomba msaada au la. Mahakama hii pia ilikataa utetezi wa Mjibu Maombi kwamba uwakilishi wa kisheria wa bila malipo unapatikana kulingana na rasilimali zilizopo kwamba hauna msingi. Mahakama iliona kuwa, kwa kushindwa kumpa Mleta Maombi uwakilishi wa kisheria bila malipo wakati wa uendeshaji wa kesi za ndani, Mjibu Maombi alikiuka Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba kama kinavyosomwa pamoja na Kifungu cha 14(3)(d) cha Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR).

Kuhusu madai ya kushindwa kuwajulisha Ubalozi wa Rwanda kuhusu kukamatwa na kufungwa kwa Mleta Maombi, Mjibu Maombi anakataa kuwa haki za Mleta Maombi kwa mujibu wa Mkataba na Katiba zilizingatiwa na kulindwa kikamilifu. Mahakama iliona kwamba ingawa Mkataba na ICCPR haviweki wazi masuala ya kibalozi, Makubaliano ya Vienna kuhusu Mahusiano ya Kibalozi (VCCR) ambayo Mjibu Maombi ni mhusika, huweka wazi. Kifungu cha 36(1) cha VCCR kinaonyesha haki za kibalozi za raia wa kigeni waliokamatwa na majukumu na wajibu wa Serikali. Iliona pia kwamba huduma za kibalozi ni muhimu kuhusiana haki ya kusikilizwa kwa haki kwa watuhumiwa raia wa kigeni. Mahakama ilibainisha kuwa Kifungu cha 36 cha VCCR kinaweka majukumu mawili kwa Serikali inayopokea, pia kinampa mfungwa haki binafsi.

Wajibu wa kwanza ni kumjulisha mfungwa raia wa kigeni haki yake ya kupata huduma za ubalozi na pili ni kuwezesha utoaji wa huduma za kibalozi ikiwa mfungwa raia wa kigeni ataomba hivyo. Wajibu wa pili

unategemea ombi kutoka kwa mfungwa, baada ya mfungwa huyo kufahamishwa kuhusu haki yake ya kupata huduma za kibalozi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kuwa kwa kushindwa kumjulisha Mleta Maombi kuhusu haki yake ya kupata huduma za kibalozi, Mjibu Maombi alimnyima fursa ya kutafuta msaada wa kibalozi ili kuwezesha utetezi wake, na hivyo kukiuka Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba kama kinavyosomwa pamoja na Kifungu cha 36(1) cha VCCR.

Kuhusu madai ya mahakama za ndani kushindwa kuzingatia ushahidi, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba "uendeshaji kesi kwa kuzingatia haki kunahitaji kwamba kutoa hukumu katika kosa la jina, na hasa, adhabu nzito ya kifungo, inapaswa kutolewa kwa misingi ya ushahidi thabiti na wa kuaminika". Mahakama hii pia iliona kwamba, katika kupitia sababu hii ya rufaa, Mahakama ya Rufaa ilizingatia ushahidi ulio kwenye rekodi, maelezo ya mwathiriwa na ushahidi wa mganga na ni kwa msingi huo, ndipo Mahakama ya Rufaa iliona kwamba mahakama iliyondesha kesi ilitoa hukumu inavyofaa kwa Mleta Maombi kutokana na kosa la ubakaji kwa sababu mwathiriwa aliingiliwa na kulikuwa na ushahidi wa kuthibitisha, vivyo hivyo iliunga mkono uamuzi wa Mahakama Kuu, kwa hivyo ikatupilia mbali rufaa ya Mleta Maombi.

Mahakama hii iligundua kwamba ingawa kulikuwa na kutofautiana kwa utaratibu kwenye mahakama iliyoendesha kesi katika kukubali ripoti ya matibabu, Mahakama Kuu iliondoa ripoti ya matibabu na kwa hivyo haikuzingatiwa wakati wa kutathmini ushahidi. Kosa hili la kiutaratibu kuhusu Mahakama Iliyoendesha Kasi kukubali ripoti ya matibabu kama ushaidi halikuonesha kosa lolote kwa udhahiri ambalo lilisababisha kuharibika kwa haki, kukihitaji Mahakama iingilie kati. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi hakuvunja haki ya Mleta Maombi kuhusu kusikilizwa kesi yake kwa haki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba na kwa hivyo ilitupilia mbali madai hayo.

Kuhusu madai kwamba kesi hiyo haikuthibitishwa bila shaka lolote, Mjibu Maombi anasema kwamba upande wa mashtaka ulitoa ushahidi na kuthibitisha kesi yake bila shaka lolote mbele ya Mahakama Iliyoendesha Kesi na ndiyo maana Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ziliunga mkono uamuzi wa Mahakama Iliyoendesha Kesi. Mahakama iliona kwamba, kutokana na kumbukumbu, upande wa mashtaka ulitegemea ushuhuda wa kuthibitisha wa mwathiriwa na mashahidi, kwa kuwa kumbukumbu ya matibabu ilifutwa na Mahakama Kuu kuwa sehemu ya ushahidi ulio kwenye kumbukukumbu. Aisha, Mahakama hii inaona kwamba Mleta Maombi hakuonyesha jinsi upande wa mashtaka ulishindwa kuthibitisha kesi yake bila shaka lolote. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi hakuvunja haki ya Mleta Maombi kuhusu kusikilizwa kesi yake kwa haki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 7 cha Mkataba na kwa hivyo ilitupilia mbali madai hayo.

Kuhusu fidia, Mleta Maombi aliomba fidia ya kifedha na isiyo ya kifedha ikiwa ni pamoja na kuachiliwa huru kutoka gerezani. Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Maombi hakuweka uhusiano wowote kati ya ukiukwaji uliobainishwa na hasara ya mali anayodai ameipata. Kwa hivyo, ilitupilia mbali madai ya Mleta Maombi kuhusu fidia ya hasara ya mali. Kwa hiyo, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mleta Maombi.

Kuhusu hasara ya kimaadili, Mahakama ilitoa jumla ya Shilingi za Tanzania Laki Tatu (TZS 300,000) kama fidia ya ukiukwaji wa aina mbili kuhusu haki ya kupata usaidizi wa kisheria bila malipo na haki ya kupata huduma za kibalozi. Mahakama pia ilimwamuru Mjibu Maombi kulipa fidia hiyo bila kutozwa kodi, ndani ya miezi sita (6), tangu tarehe ya kutolewa taarifa ya Hukumu hii, akishindwa kufanya hivyo, Serikali itatakiwa kulipa riba ya malimbikizo ya madeni yanayokokotolewa kwa msingi wa kiwango kinachotumika cha Benki Kuu ya Tanzania katika kipindi chote cha kucheleweshwa kwa malipo hadi kiasi chote kitakapolipwa kikamilifu.

Kuhusiana na fidia zisizo za kifedha, kuhusu maombi ya Mleta Maombi kwamba hatia na hukumu yake vitupiliwe mbali na atolewe gerezani, Mahakama ilibaini kwamba hakuonesha ushahidi wa kutosha, wala Mahakama haikubainisha kwamba hatia na hukumu yake ilitokana na mazingatio yasiyo ya mantiki na kwamba yenye kuendelea kubaki gerezani ni kinyume cha sheria. Kwa hivyo ilitupilia mbali maombi hayo. Kuhusu maombi kwamba ukiukwaji uliofanywa dhidi yake usirudiwe, Mahakama iliona kwamba ukiukaji huu haukuwa wa kimfumo kwa asili, aidha, hakuna ushahidi kwamba ukiukwaji huu umerudiwa au unaweza kurudiwa. Kwa hiyo mahakama ilitupilia mbali maombi haya.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake mwenyewe.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0582016

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*